## KUPANDA BEI YA MAFUTA

# LATRA yaonya watoa huduma ya usafiri

NA MWANDISHI WETU

BEI ya mafuta ya petroli imepanda kwa kiwango kikubwa ambapo kwa jiji la Dar es Salaam, imepanda kutoka shilingi 2,864 kwa lita mwezi Machi hadi shilingi 3,820 kwa lita mwezi Aprili 2026, kulingana na taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). .

Taarifa hiyo inaeleza kuwa kupanda kwa bei kunatokana na mabadiliko ya soko la kimataifa, likiwemo ongezeko la bei ya mafuta ghafi na changamoto za usafirishaji.

Aidha, hali ya kisiasa na kiusalama duniani, hususan mvutano unaoendelea kati ya mataifa mbalimbali, imechangia kuvuruga upatikanaji na usambazaji wa mafuta katika masoko ya kimataifa.

Kwa mujibu wa EWURA, gharama za uagizaji na usafirishaji zimeongezeka, zikichangiwa pia na kupanda kwa gharama za bima ya meli pamoja na ucheleweshaji wa mizigo.

Hali hii imepelekea bei za rejareja kupanda katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, ambako bei mpya zimeanza kutumika rasmi kuanzia jana Aprili mosi mwaka huu.

Kutokana na ongezeko hilo, wananchi wametakiwa kutumia nishati kwa uangalifu na kuzingatia mbinu mbadala ili kupunguza gharama.

Serikali kupitia EWURA imeeleza kuwa itaendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mafuta duniani na kuchukua hatua stahiki kulinda maslahi ya watumiaji wa kawaida.

Wakizungumza na Zanzibar Leo, baadhi ya wananchi, waliomba serikali kuangalia uwezekano wa kutoa ruzuku ili kupunguza ukali wa bei ya mafuta ambao utasababisha bei za bidhaa nyengine ikiwemo chakula kupanda.

"Hii haijawahi kutokea katika miaka ya karibuni, hatujawahi kushuhudia bei ya lita moja ya petroli au dizeli kupanda kwa zaidi ya shilingi 1,000, tunaiomba serikali ifirike kutoa ruzuku," alisema Paul Richard wa Kariakoo.

Kwa upande wake, Fatuma Salumu, wa Mwenge, alisema ana wasiwasi mkubwa bei za bidhaa za chakula zitapanda mara dufu kwa sababu gharama za usafirishaji wa mchele kutoka Ifakara zitaongezeka.

Kwa upande wake, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewaonya watoa huduma za usafirishaji kutotumia kigezo cha kupanda bei za mafuta kuwaumiza wananchi kwa kuwapandishia nauli kiholela.

Aidha, mamlaka hiyo imeitisha kikao cha dharura na watoa huduma kinachotarajiwa kufanyika Aprili 8 na kuwataka wahusiha kushiriki ili wajadili namna bora ya kuvuka katika kipindi hiki.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Saluo, alitoa kauli hiyo jana Kibaha mkoani Pwani, kwenye semina na waandishi wa habari.

"Ninawaomba wasafirishaji wasitumie nafasi ya kupanda bei za mafuta kuwaumiza Watanzania, hiki ni kipindi cha mpito, wasipandishe nauli bila mwongozo wa LATRA," alisema.

Mapema akiwasilisha hotuba ya bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu bugeni jijini Dodoma, Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema licha ya kuwepo changamoto za kisiasa na kiusalama katika Mashariki ya Kati, serikali itaendelea kusimamia bidhaa za mafuta ili kuhakikisha zinaendelea kuwa himilivu.

"Tumeona bei zimeanza kupanda, serikali itakaa kuhakikisha tunakabiliana na tatizo hilo ili wananwanchi waendelee kupata bidhaa ya mafutwa kwa bei watakayoweza kuimudu na kudhibiti kupanda kwa gharama za maisha," alisema.

Alisema serikali imeendelea kusimamia mifumo ya kuagiza na kusambaza mafuta pamoja na kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi bidhaa hiyo katika bandani za Dar es Salaam na Mtwara.

# Latra yazuia kupandisha nauli

**Na Ikunda Erick, Kibaha**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeagiza watoa huduma za usafiri wasipandishe nauli kiholela.

Baadhi ya mabasi na daladala yameanza kuongeza nauli baada ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kutangaza ongezeko la bei za mafuta ya dizeli na petroli.

Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Habib Suluo alisema mamlaka hiyo inatambua changamoto zinazowakabili wasafirishaji watoa huduma lakini mabadiliko yoyote ya nauli lazima yafanyike kwa kuzingatia sheria na kanuni.

"Hatutaruhusu ongezeko holela la nauli. Lazima utaratibu ufuatwe ili kulinda maslahi ya wananchi," alisema Suluo katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere Kibaha mkoani Pwani jana.

Alitangaza kuitisha kikao cha wadau Aprili 8, mwaka huu mkoani Dar es Salaam ili kujadili hali hiyo na kupata suluhisho la pamoja litakalozingatia pande zote.

Suluo alisema kwa mujibu wa sheria nauli hupangwa na Latra, kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya mamlaka hiyo na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika baada ya siku 14.

Alisema watoa huduma wanaotaka kupandisha nauli wanapaswa kuwasilisha maombi yakionesha mwenendo wa biashara zao ikiwa ni pamoja na hesabu zilizokaguliwa kwa miaka mitatu mfululizo, taarifa za uwekezaji na vielelezo vya hasara wanazopata.

Suluo alisema Latra itaendelea kushirikiana na Ewura kufuatilia mwenendo wa bei za mafuta ili kubaini athari zake katika sekta ya usafiri.

Latra ilisema itaendelea kusimamia sekta ya usafiri ili kuhakikisha wananchi hawabebeshwi mzigo wa gharama na akawaeleza wasafirishaji serikali ipo tayari kuwasikiliza.

"Ila lazima mfuate sheria lakini pia waoneeni huruma wananchi na Watanzania, msitumie changamoto iliyopo ya vita vinavyoendelea Mashariki ya Kati kujinufaisha," alisema Suluo.

# LATRA: Marufuku kupandisha nauli

Na SUPERIUS ERNEST

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewataka wadau wa usafirishaji kutopandisha nauli kiholela.

Pia, imetoa onyo watakaobainika kupandisha bei ya bidhaa hiyo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

LATRA imeitisha kikao cha dharura na wadau wa usafirishaji kitakachofanyika Dar es Salaam, Aprili 8 mwaka huu, kufanya marejeo ya nauli.

Akizungumza jana, Kibaha, Pwani, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisena baadhi ya wasafirishaji wamepandisha nauli kinyume na utaratibu.

Suluo aliwataka wasafirishaji na wananchi kuwa watulivu kipindi hiki ambapo LATRA na wadau hao wanatajiwa kukutana kujadili suala hilo.

Alisema ni mara ya kwanza viwango vya nauli kupanda kwa kiasi kikubwa baada ya EWURA jana kutangaza bei mpya ya bidhaa hiyo.

Taarifa ya EWURA ilisema Mkoa wa Dar es Salaam bei elekezi na rejereje ya petroli ni sh.3,820, dizeli sh.3,806 na mafuta ya taa sh. 3,881.

Mkoa wa Tanga bei elekezi na rejareja sh.3,881, dizeli sh.3,867 na mafuta ya taa sh. 3,745. Mtwara petroli sh. 3,912, dizeli sh. 3,898 na mafuta ya taa sh. 3,777.

Pia, EWURA ilitoa bei kikomo za mafuta hayo, ambapo Dar es Salaam petroli sh. 3,677.71, dizeli sh. 3,663.29 na mafuta ya taa sh. 3,542.70.

Mkoa wa Tanga bei za kikomo petroli sh. 3,685.00, dizeli sh. 3,659.26 na Mtwara petroli sh. 3,669.32 na dizeli sh. 3,669.98.

Taarifa ya EWURA ilisema sababu ya ongezeko la bei hiyo ni vita inayoendelea Mashariki ya Kati iliyosababisha kushambuliwa visima vya mafuta, ghala la kuhifadhiwa mafuta na viwanda vya kusafisha mafuta.

Pia, Iran kufunga lango la Hurmuz linalopitisha takribani asilimia 20 ya mafuta yanayosafirishwa kwenda masoko mbalimbali duniani.

Taarifa hiyo ilisema, Tanzania inaagiza kwa kiasi kikubwa mafuta kutoka Mashariki ya Kati, hivyo vita hiyo imesababisha kuongeza gharama za usafirishaji wa bima za meli za mizigo ikiwemo mafuta.

# LATRA warns against arbitrary fare hikes

By DAILY NEWS Reporter

THE Land Transport Regulatory Authority (LATRA) has instructed transport operators across the country to refrain from arbitrarily hiking fares during the current transition period, despite the recent rise in fuel price.

The authority urged operators to adhere to established legal procedures, as it continues to monitor operational costs.

LATRA also provided a seven-day window to convene a stakeholders' meeting aimed at reviewing areas that may require fare adjustments, if deemed necessary.

The move comes a day after the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) announced an increase in fuel prices by more than 900/- per litre from 2864 to 3820.

The sharp rise in fuel prices has been linked to the ongoing tensions in the Middle East involving the United States, Israel and Iran.

Speaking yesterday during press briefing in Kibaha, Coast Region, LATRA Director General, Habibu Suluo, said the authority has received complaints from members of the public over some service providers increasing fares without approval, contrary to laid down procedures.

"We cannot allow fare adjustments to be implemented outside the legal framework," he stressed.

He noted that the authority has scheduled a stakeholders' meeting on April 8 this year to deliberate on the matter.

According to him, the meeting will bring together service providers, consumers and other key stakeholders, and will also be broadcast live to enable wider participation, including those unable to attend physically.

"Any fare review will be conducted in line with existing regulations, including an assessment of return on investment, which should remain below 10 per cent within a period of not less than three years," he said.

He further called on service providers with concerns over rising operational costs to submit supporting documents to justify their claims for consideration in accordance with the law.

CPA Suluo stressed that until an official decision is reached, no operator is permitted to increase fares, warning that any violation will attract legal action.

LATRA has also urged all stakeholders to actively participate in the upcoming meeting and submit their proposals on time to ensure a balanced outcome that considers the interests of all parties.

He added that the authority reserves the right to use its own data to make fare determinations should operators fail to submit the required information as stipulated under LATRA regulations.

## Govt moves to

MABADILIKO YA BEI ZA BIDHAA




Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura)

# Bei za mafuta zaanza kung'ata

Aurea Simtowe na Habel Chidawali, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dar/Dodoma. Sasa si hadithi tena ni rasmi kwamba, bei za mafuta ya petroli na dizeli nchini na nchi majirani zimeanza kung'ata kutokana na kupaa kwa kasi.

Kupanda kwa gharama hizo kuanzia jana Aprili mosi, 2026 kunatajwa kuwa pigo kwa wananchi na shughuli za kiuchumi, huku athari zake zikianza kujitokeza haraka katika maisha ya kila siku.

Ongezeko hilo la zaidi ya Sh900 lililotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura), linaelezwa kuchochewa na mgogoro wa kimataifa unaoendelea kati ya Marekani na Israel dhidi ya Iran, uliioanza Februari 28, 2026.

Mgogoro huo umeathiri uzalishaji na usafirishaji wa mafuta ghafi duniani, hasa baada ya kufungwa kwa Mlango wa Hormuz ambao hupitisha takribani asilimia 20 ya mafuta yote yanayosafirishwa duniani.

Vilevile, kushambuliwa kwa visima vya mafuta, maghala ya kuhifadhi mafuta na viwanda vya kuyasafisha kumeigusa moja kwa moja Tanzania ambayo inaagiza mafuta kwa kiasi kikubwa, jambo linalotajwa kuongeza gharama za usafirishaji kutokana na kukosekana kwa meli za kuyasafirisha.

Katika mazingira hayo, mzigo mkubwa unaangukia kwa watumiaji wa mwisho. Gharama za usafiri zimeanza kupanda, sambamba na bei za bidhaa na huduma, huku wafanyabiashara wakikabiliwa na ongezeko la gharama za uzalishaji.

Saa chache baada ya Ewura kutangaza bei mpya, watoa huduma za usafiri wakiwamo bodaboda, bajaji na daladala wameanza kupandisha nauli. Hatua hiyo imezidisha maumivu ya wananchi wanaokabiliwa na gharama kubwa za maisha.

Taarifa zinaonyesha kuwa bei za petroli na dizeli zimeongezeka kwa zaidi ya Sh900 kwa lita, ikiwa ni ongezeko kubwa ambalo halijashuhudiwa kwa muongo kadhaa sasa.

Kutokana na ongezeko hilo, Rashid Said aliyejaza tanki lake la gari kwa lita 45, amelipa takriban Sh40,000 zaidi ya kiwango alichokuwa analipa kwa bei za Machi ambazo zimekoma jana.

Mbali na Said, vilio vingine vya bei kung'ata vilianza kusikika jana hiyo kwenye nauli za daladala, bajaji na bodaboda.

Kutokana na hali hiyo, Chama cha Kampuni za Uuzaji Mafuta Tanzania (Taomac) kimeonya kuwa mwelekeo wa bei unaweza kuendelea kupanda katika miezi ijayo, kikitaka wananchi kujiandaa kukabiliana na hali hiyo.

Kwa upande wake, Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (Tamstoa) kimeishauri Serikali kutafakari upya tozo mbalimbali za mafuta ndani ya muda mfupi, ili kupunguza makali ya bei kwa watumiaji.

Wakati huohuo, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa) kimeomba mamlaka husika kuruhusu ongezeko la nauli haraka, kikionya kuwa bila hatua hiyo, wamiliki wa mabasi wanaweza kuingia hasara kubwa.

Hoja hiyo inaungwa mkono pia na wamiliki wa daladala, ambao wamesisitiza umuhimu wa kupitia upya viwango vya nauli ili kuendana na uhalisia wa gharama mpya za uendeshaji.

### Onyo ongezeko la nauli

Katikati ya hoja hizo za wasafirishaji, Mamlaka ya Udhibiti wa usafiri Ardhini (Latra) imeonya upandishaji holela wa nauli usiofuata utaratibu huku ikipanga kuitisha kikao cha wadau.

Mwangwi wa ongezeko hilo ulifika pia bungeni jijini Dodoma, ambapo Spika Bunge, Mussa Zungu alitoa maelekezo kwa Serikali juu ya suala hilo huku Waziri Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba akisema Serikali itaangalia uwezekano wa kuleta unafuu kwa Watanzania.

### Bei zenyewe

Katika bei zilizotangazwa jana wananchi wa Kyerwa mkoani Kagera ndio watakaoingia zaidi mfukoni wakitakiwa kulipa Sh4,092 kwa lita moja ya petroli na Sh4,078 kwa dizeli.

Mbali na hilo, sasa watumiaji wa mafuta yanayopitia Bandari ya Dar es Salaam watalazimika kuongeza Sh956 katika kila lita moja ya petroli baada ya bei hadi Sh3,820 badala ya Sh2,864 za mwezi uliopita.

Kwa upande wa dizeli, lita moja sasa wataitumia kwa Sh3,806 kutoka Sh2,858 ikiwa ni ongezeko la Sh948. Mafuta ya taa sasa watayanunua kwa Sh3,684 badala ya Sh2,932 za awali, sawa na ongezeko la Sh752.

Kwa upande wa watumiaji wa petroli iliyopitia Bandari ya Tanga wao watapata lita moja kwa Sh3,881 kutoka Sh2,925 ikiwa ni ongezeko la Sh956 huku dizeli wakiipata kwa Sh3,867 badala ya Sh2,919 ya Machi mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la Sh948.

Watumiaji wa mafuta ya taa watalazimika kuongeza Sh752 kwa kila lita kufikia Sh3,745 kutoka Sh2,993.

Kwa mafuta yaliyoingiia Mtwara wao watatumia Sh3,912 kupata lita moja ya petroli ikiwa ni ongezeko la Sh956 kutoka bei iliyokuwapo Machi, dizeli Sh3,898 badala ya Sh2,951 ikiwa ni ongezeko la Sh947 huku mafuta ya taa yakifikia Sh3,777 kwa lita kutoka Sh3,025.

> "Tunafahamu gharama zimeongezeka, ila haiwezekani kwa mtoa huduma kuamka na kuongeza nauli au kusimamisha usafiri bila kufuata kanuni, tunahitaji utulivu katika sekta."
>
> Habibu Suluo

> "Pia watu binafsi wanaweza kupunguza mahitaji kwa kuchangia magari kwa kuwa hii ni changamoto kubwa inayohitaji jitihada za pamoja katika kuitatua."
>
> Raphael Mgaya

### Vipi kuhusu akiba ya mafuta

Hayo yamejiri licha ya Machi 27, 2026, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati anayeshughulikia Mafuta na Gesi, Dk James Mataragio kueleza Tanzania ina akiba ya mafuta yanayoweza kutumika kwa miezi mitatu.

Alisema petroli yaliyopo nchini kwenye matenki ni lita 95.25 milioni, yaliyowasili nchini ni lita 146.68 milioni, yaliyopo njiani ni lita 138.73 milioni ambayo kwa jumla yanatosha kwa matumizi ya siku 61 hadi Juni 2026.

Alisema mikataba ya mafuta iliyoingiwa na mzabuni ni jumla ya lita 183.5 milioni ambayo yatafika nchini mwezi wa Aprili, hivyo jumla ya mafuta ya petroli yaliyopo kwenye matenki, yatakayowasili nchini kwa meli pamoja na yaliyopo kwenye mikataba ni lita 563,682,461 kiasi ambacho kinatosha kwa siku 91.

Kwa upande wa dizeli iliyopo kwenye matenki ni lita 55.74 milioni, iliyowasili ni lita 122.89 milioni, iliyopo njiani ni lita 184.66 milioni na kufanya jumla ya lita 362.43 milioni yanayotosha kwa matumizi ya siku 44.

Mafuta ya dizeli yaliyopo kwenye mikataba na wazabuni ni lita 167.32 milioni kwa ujumla, mafuta yaliyopo nchini yanayokuja kwa meli na yaliyopo kwenye mikataba ni lita 530,621 milioni kiasi kitakachotosheleza kwa siku 64.

Jana Aprili 1, 2026, Kamishna Mafuta na Gesi wa Wizara ya Nishati, Goodluck Shirima alifafanua: "Tunaposema tuna akiba ya mafuta, haimaanishi kwamba mafuta yote yapo ndani ya nchi kwenye matenki yetu pekee."

"Akiba hiyo inajumuisha mambo kadhaa, mafuta yaliyopo nchini, yale yaliyopo njiani yakiletwa kwa meli, pamoja na mikataba tuliyoingia na makampuni ya kusambaza mafuta," alisema Shirima.

Shirima alisema kampuni hizo hununua mafuta kutoka kwenye soko la dunia na bei ya mafuta nchini hupangwa kulingana na gharama za ununuzi katika soko hilo.

"Reference ya bei ya mafuta yanayouzwa chini ni utaratibu wa bei wa M-1, hivyo mafuta yanayouzwa mwezi Aprili, bei zake katika soko la dunia za Machi, mafuta yatajayouzwa Mei yanakuwa yamenunuliwa kwenye soko la dunia kwa bei za Aprili."

Licha ya ufafanuzi huo, mtaalam mmoja wa mafuta alisema kinachojadiliwa ni bei ya mafuta sio ujazo uliopo nchini, akidokeza kuna sababu nyingine ya ongezeko la bei kwa kuwa mafuta yanayouzwa sasa yaliingia nchini mwezi Februari kabla ya vita.

### Kauli ya Serikali, Bunge

Akiwasilisha makadirio ya bajeti ya ofisi yake kwa mwaka 2026/27 jana, Waziri Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba alisema:

"Tumeona bei zimeshaanza kupanda, tutakaa ndani ya Serikali kuhakikisha tunakabiliana nalo vipi suala hili ili wananchi waendelee kupata mafuta kwa bei nzuri na kudhibiti kupanda kwa gharama za maisha."

Hata hivyo, Dk Mwigulu alisema licha ya changamoto zinazoendelea Mashariki ya Kati, Serikali itaendelea kusimamia upatikanaji wa petroli na dizeli ili kuhakikisha zinaendelea kuwa himilivu.

Katika hatua nyingine, Dk Mwigulu Serikali alisema Serikali itaendelea kusimamia mifumo ya kuagiza, kuhifadhi na kusambaza mafuta pamoja na kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Mtwara.

Kwa mujibu wa Dk Mwigulu, katika kufanikisha hilo Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa ghala la kupokea na kuhifadhi mafuta lenye uwezo wa kupokea tani 308,110 katika Bandari ya Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 30.

Baada ya maelezo hayo, Spika Zungu, alimuagiza Waziri wa Nishati, Deogratias Ndejembi kukutana na Kamati ya Bunge ya Nishati ili kujadili hali na mwenendo wa kupanda kwa bei hizo.

Zungu alisisitiza bila upatikanaji wa uhakika wa mafuta, utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo unaweza kukwama.

### Onyo la Latra

Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Habibu Suluo aliwataka wasafirishaji kuacha kupandisha nauli na wafuate utaratibu uliowekwa kabla ya kufanya mabadiliko yoyote, akisisitiza ongezeko lisiloidhinishwa linaweka mzigo usio wa haki kwa abiria.

Alisema pamoja na kupanda kwa mafuta, watoa huduma wanapaswa kuendelea kutoa huduma bila kusitisha safari wala kuongeza nauli bila kibali.

"Tunafahamu gharama zimeongezeka, lakini haiwezekani kwa mtoa huduma kuamka na kuongeza nauli au kusimamisha usafiri bila kufuata kanuni, tunahitaji utulivu katika sekta hii," alisema Suluo.

Alisema mabadiliko ya nauli hufuata utaratibu maalumu uliowekwa kisheria, akitaja mtoa huduma anayetaka kupandisha nauli anatakiwa kuwasilisha maombi rasmi kwa Latra kwa mujibu wa kanuni za mamlaka hiyo.

Suluo alisema katika mchakato huo, mambo kadhaa huzingatiwa ikiwemo gharama za uendeshaji wa huduma, matengenezo na mishahara, kiwango cha uwekezaji kilichowekwa na mtoa huduma, mrejesho wa uwekezaji, hali ya uchumi na uwezo wa wananchi kumudu nauli, ushindani wa soko na upatikanaji wa huduma.

Aidha, alisema Latra imepanga kukutana na wadau wa sekta ya usafiri Aprili 8, mwaka huu jijini Dar es Salaam ili kujadili kwa pamoja athari za kupanda kwa bei ya mafuta na kupata maoni kabla ya kufanya uamuzi wowote kuhusu nauli.



### Watanzania wajiandae

Wakati hali ikiwa hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Taomac, Raphael Mgaya amedokeza bei za mafuta zitakwenda kupanda zaidi, hivyo akawataka wananchi kujiandaa kisaikolojia.

Alisema bei ya sasa ni nafuu kwani kuna mafuta ambayo hado yalikuwapo nchini, tofauti na kipindi ambacho mafuta yatakayoanza kutumika yatakuwa ni yale yanayoingia.

"Mwezi ujao bidhaa zote zitakuwa ghali, bei zitaongezeka zaidi, haijawahi tokea katika sekta ya mafuta hali kama hii na imetokana na mapigano yanayoendelea katika nchi zinazozalisha mafuta, hivyo ni suala la watu kujiandaa kisaikolojia," alisema.

"Tujiandae kwa sababu haikuwepeki kwani hata miundombinu ya kuzalisha, kusafisha, hadi uzalishaji kurejea katika hali yake ya kawaida itachukua muda," alisema.

Kuhusu namna ya kushughulikia suala hilo, alisema kodi zinaweza kuangaliwa ili kutoa unafuu fulani lakini hata zikitolewa, bado mafuta yataendelea kuwa juu.

"Bei zinavyopanda ukitoa kodi itasaidia lakini hutapunguza maumivu yote kwa sababu kodi ni kama asilimia 30 kutegemeana na bei husika," alisema.

Alisema suala hili kwa sasa linahitaji jitihada za pamoja katika kuitafutia ufumbuzi huku akipendekeza kwa taasisi ambazo watu wanaweza kufanyia kazi nyumbani, waruhusiwe ili kupunguza mahitaji na matumizi ya mafuta.

"Pia watu binafsi wanaweza kupunguza mahitaji kwa kuchangia magari kwa kuwa hii ni changamoto kubwa inayohitaji jitihada za pamoja katika kuitatua," alisema.

Mbali na hilo, alisema ni vyema kudhibiti ulanguzi wa mafuta kwa kuwa katika hali kama hii watu wanaweza kuwa tayari kutunza mafuta majumbani kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

FAHAMU >

## Bei za mafuta kwingineko katika nchi jirani

Kenya lita moja inauzwa kwa KSh178.28 sawa na Sh3,549.16 kwa petroli na KSh166.54 sawa na Sh3,315.44 kwa dizeli huku kukiwa na vilio vya upatikanaji kutokana na kinachoelezwa kuwa wafanyabiashara wameficha.

Uganda lita moja ya Petroli ni Uganda USh5,800 sawa na Sh4,033.94 na dizeli USh5,300 sawa na Sh3,686.18 na wanasema mafuta yapo ya kutosha hadi Mei, 2026.

Zambia mafuta yamefikia Kwacha 29.78 kwa petroli sawa na Sh4002.42 na Kwacha 27.15 Sawa na Sh3,648.95 kwa dizeli.

Burundi makadirio ya bei ni Dola 1.35 sawa na Sh3,496.50 kwa petroli na dola 1.32 sawa na Sh3418.80 kwa dizeli lakini tatizo kubwa ni upatikanaji.

Afrika kusini Serikali imelazimika kupunguza ushuru wa mafuta kwa Rand 3 (Sh463.48) kwa lita moja baada ya bei yake ya mafuta kupanda kwa asilimia 15 petroli na asilimia 40 dizeli.

### Wamiliki wa mabasi, daladala

Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Priscus John alisema nauli za mabasi zinatakiwa kupandishwa haraka, vinginevyo wamiliki wa mabasi watafilisika.

Alisema kabla ya bei ya mafuta kutangazwa bidhaa nyingine ikiwemo vipuri vilikuwa zimeongezeka bei na mara zote wauzaji wanalalamika kuwa bei zimeongezeka kutokana na vita Mashariki ya Kati.

"Vita vimeshaanza kupanda, ukiguisa spea ni ama hazipatikani au bei zimepanda," alisema.

Alisema kufuatia ongezeko hili sasa gari linalofanya safari kwenda na kurudi kwa lita 900, gharama zake zimeongezeka kwa Sh800,000 kwa siku.

### Wamiliki wa daladala

Katibu wa Chama cha Wamiliki wa Daladala Mkoa wa Dar es Salaam, Shifaya Ansselema alisema bei mpya inaathiri nchi nzima kwani hakuna jambo ambalo halina mazungumzo.

Alisema anaamini taasisi za Serikali zinaona na mamlaka za udhibiti Ewura na Latra zinaona, hivyo ni vyema kuhakikisha sekta zote zinaendelea kustawi.

"Tunaamini katika mazungumzo, hatuangalii mafuta tu, vilainishi vimepanda muda mrefu, tukikaa tuangalie tunaendaje na hali hii kama itaendelea, tukikaa kwenye meza ya mazungumzo tunaweza kuelewana," alisema.

Alisema ni vyema wananchi na wamiliki wa magari waendelee na shughuli zao wakati wakitafuta namna ya kuzungumza na Serikali ili kujua namna ya kukabiliana na hali hii.

### Wamiliki wa malori

Kilio kama hicho, kilitolewa na Chuki Shabani, mwenyekiti wa Tamstoa, akitaka vyema Serikali iangalie namna ya kupunguza tozo katika mafuta ili kupunguza makali ya bei.

"Hii haitaathiri tu sisi wafanyabiashara, bali hadi wamiliki wa magari binafsi, wanaotumia vyombo hivyo kama nyenzo ya usafiri na si kwa faida," alisema.

"Kwa wafanyabiashara anaweza kusema utaongezea kwa mlaji lakini kwa wakulima, madaktari inawahusu moja kwa moja kwa sababu hawapati faida. Serikali ipunguze tozo zilizopo kwenye mafuta kwani zipo zaidi ya nane," alisema.

### Nauli juu

Kabla ya hatua zozote kufanyika zinazoadhinisha ongezeko la bei tayari wananchi wameanza kuugulia maumivu ya athari hiyo kutokana na kulipa nauli zaidi ya waliyokuwa wakilipa awali.

Nauli hizo zimeongezeka kwa wastani wa Sh500 katika kila safari ya bodaboda na bajaji wakati ambao wamiliki wa mabasi wakitaka mamlaka zinazohusika ziangalie namna ya kupandisha bei ili wasifirisike.

Kwa watumiaji wa bajaji kati ya Goba Center hadi Mlimani City, Dar es Salaam ambao walikuwa wakilipa Sh2,000 jana walilazimika kulipa Sh2,500 kuhu nauli kutoka Mlimani City hadi Mwananchi wakilazimika kulipa Sh1,500 badala ya Sh1,000.

Kwa watu wanaotoka Mbezi hadi Njia Panda ya Chuo sasa wanalipa Sh2,600 kutoka Sh2,000 na wanaofika Mwenge wakilipa Sh3,000 badala ya Sh2,500. Kutoka Kinyerezi hadi Mbezi ilikuwa Sh1,000 lakini sasa ni Sh1,500.

"Bei lazima ziongezeke kwa sababu mafuta yamepanda, vinginevyo ni ngumu kuona faida ya kile unachokifanya," alisema Manase Msakula dereva wa bajaji.




Malori yakiwa yameegeshwa kwenye Kituo cha Mafuta cha Camel Tabata, Dar es Salaam huku bango la bei ya mafuta likionyesha kupanda kwa nishati hiyo.
Picha na Michael Matemanga

NISHATI

# Bei za mafuta zatikisa

Na Waandishi Wetu

KUPANDA kwa bei za mafuta nchini kumeshtua wananchi na wadau wa uchumi, huku maswali makubwa yakielekezwa kwa serikali kuhusu uhalali wa ongezeko kubwa licha ya kuwapo akiba ya kutosha ya mafuta.

Bei mpya za mafuta zilizotangazwa jana zimeibua mjadala, zikitajwa zitaumiza mifuko ya Watanzania, hali iliyosababisha baadhi ya wananchi kuhoji kwa nini ongezeko hilo linatokea wakati serikali imekuwa ikisisitiza kuwa nchi ina akiba ya mafuta ya zaidi ya miezi mitatu.

Wakati sintofahamu hiyo ikiendelea, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imeonya vikali watoa huduma za usafiri dhidi ya kupandisha nauli kiholela.

Mamlaka hiyo imesisitiza kuwa hakuna mabadiliko ya nauli yatakayokubalika bila kufuata taratibu rasmi.

Hata hivyo, katika hali inayoonyesha shinikizo la moja kwa moja la gharama, baadhi ya waendesha daladala, bajaji na bodaboda wameanza kupandisha nauli kinyemela, hatua inayowaumiza zaidi wananchi wa kipato cha chini wanaotegemea usafiri huo kwa maisha ya kila siku.

Bungeni jijini Dodoma, nako wabunge wameibua hoja nzito wakitaka maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa bei za mafuta, huku wakionya kuwa hali hiyo inaweza kuathiri mipango ya maendeleo na ustawi wa wananchi.

Bunge limeiagiza serikali kuchukua hatua za haraka, ikiwamo kutoa ufafanuzi na kuweka mikakati ya kudhibiti athari za ongezeko hilo.

Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba amesema serikali inaendelea kutafuta suluhu ya kudumu, ikiwamo kupunguza utegemezi wa mafuta kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kama gesi asilia.

Pia ameagiza maandalizi ya miundombinu na sera zitakazowezesha magari ya serikali kutumia gesi ili kupunguza gharama za uendeshaji.

**RIPOTI KAMILI**

Bunge limeiagiza serikali kutoa maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa bei za mafuta nchini kufuatia kupanda kwa ghafla kwa gharama za nishati hiyo, hatua iliyozua maswali na wasiwasi miongoni mwa wabunge na wananchi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Spika wa Bunge, Mussa Zungu, akimtaka Waziri wa Nishati, Deogratius Ndejembi, kukutana na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ili kujadili kwa kina sababu za ongezeko hilo, gharama halisi na hali ya upatikanaji mafuta.

Hatua hiyo inafuatia tangazo la bei elekezi mpya kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) zilizoanza kutumika jana, Aprili Mosi, 2026, zikionesha ongezeko la takribani asilimia 33, hali inayotishia kuongeza gharama za maisha na uzalishaji.

"Bila mafuta, shughuli nyingi za kiuchumi na mipango ya taifa zinaweza kukwama. Ni lazima tupate ufafanuzi wa kina," Spika Zungu alisisitiza, akiongeza kuwa baada ya kikao hicho, serikali itawasilisha taarifa rasmi bungeni.

**KAULI YA SERIKALI**

Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha hotuba bungeni jana, alisema serikali inaendelea kutafuta suluhu za muda mfupi na mrefu kukabiliana na changamoto ya kupanda kwa bei ya mafuta, akitaja athari za migogoro ya kimataifa, hususan katika ukanda wa Mashariki ya Kati, kuwa miongoni mwa visababishi vikuu.

Alisisitiza kuwa licha ya mazingira hayo magumu, serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji mafuta unakuwa wa uhakika na bei zinabaki himilivu kadri inavyowezekana.

Katika mkakati wa kupunguza utegemezi wa mafuta, Waziri Mkuu aliagiza Wizara za Ujenzi na Nishati kuandaa viwango vitakavyowezesha magari ya serikali kutumia gesi asilia iliyosindikwa, hatua inayolenga kupunguza gharama na kulinda uchumi dhidi ya misukosuko ya soko la dunia.

"Tunayo rasilimali ya gesi ambayo inaweza kuwa mbadala imara. Tukiiwekeza ipasavyo, hatutaathirika sana na mabadiliko ya kimataifa," alisema.

Sambamba na hilo, alisema serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mafuta. Mradi wa ghala la mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam wenye uwezo wa kuhifadhi tani 308,110 umefikia asilimia 30 ya utekelezaji, huku Bandari ya Mtwara ikiongeza uwezo wake hadi tani 110,221, hatua itakayorahisisha upokeaji shehena kubwa zaidi.

**HOJA ZAIBULIWA**

Hata hivyo, maswali yaliendelea kuibuka. Mbunge wa Tunduru Kaskazini (ACT-Wazalendo), Ado Shaibu, alihoji mantiki ya ongezeko hilo kubwa la bei, akisema halilingani na maelezo ya serikali kuwa nchi ina akiba ya mafuta ya zaidi ya miezi mitatu.

"Hili ongezeko la Sh. 1,000 kwa lita linatokana na mafuta yapi? Kama ni yaleyale yaliyokuwapo, kwa nini bei imepanda kiasi hiki?" alihoji.

Hoja hii ndiyo imetawala katika mitandao mingi ya kijamii nchini.

Ado ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), alionya kuwa mzigo huo unaathiri moja kwa moja wananchi.

Alisisitiza kuwa iwapo serikali haitatoa majibu ya kuridhisha, wabunge wako tayari kutumia taratibu za kibunge kulazimisha mjadala mpana wa suala hilo.

Alipendekeza serikali ipunguze baadhi ya tozo katika kipindi hiki cha mpito ili kupunguza makali ya ongezeko hilo kwa wananchi.

**BEI MPYA**

Kwa mujibu wa EWURA, bei kikomo ya petroli jijini Dar es Salaam imepanda kutoka Sh. 2,864 hadi Sh. 3,820 kwa lita, ongezeko la Sh. 956. Dizeli imeongezeka kutoka Sh. 2,858 hadi Sh. 3,806, huku mafuta ya taa yakipanda kutoka Sh. 2,932 hadi Sh. 3,684.

Mabadiliko hayo pia yamegusa mikoa mingine. Arusha, petroli inauzwa Sh. 3,929 kwa lita, Dodoma Sh. 3,899, huku Geita ikiongoza kwa bei ya juu ya Sh. 4,020 kwa lita. Moshi (Kilimanjaro) nayo imefikia Sh. 3,914 kwa petroli.

Katika mkakati wa kupunguza utegemezi wa mafuta, Waziri Mkuu aliagiza Wizara za Ujenzi na Nishati kuandaa viwango vitakavyowezesha magari ya serikali kutumia gesi asilia iliyosindikwa, hatua inayolenga kupunguza gharama na kulinda uchumi dhidi ya misukosuko ya soko la dunia.

EWURA imeeleza kuwa kupanda huko kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na mivutano ya kimataifa, hususan vita kati ya Marekani kwa kushirikiana na Israeli dhidi ya Iran.

Mashambulizi kwenye miundombinu ya mafuta na kufungwa kwa Lango la Hormuz, njia muhimu inayopitisha takribani asilimia 20 ya mafuta duniani, yameathiri uzalishaji na usambazaji nishati, na hivyo kuongeza gharama za mafuta kimataifa.

Vilevile, gharama za usafirishaji na bima ya meli zimepanda, hali inayochangia zaidi ongezeko la bei. Mamlaka hiyo imesisitiza kuwa hali hiyo ni ya kidunia, na Tanzania inaendelea kuchukua hatua kuhakikisha upatikanaji mafuta unabaki wa uhakika huku bei zikidhibitiwa kadri inavyowezekana.

**WANANCHI**

Pamoja na maelezo hayo, wananchi wengi wameibua maswali, hasa kuhusu uhalali wa ongezeko hilo wakati serikali ilitangaza kuwa nchi ina akiba ya mafuta ya kutosha kwa miezi mitatu.

Kupitia mitandao ya kijamii, baadhi ya wananchi wameonesha kutoridhishwa na maelezo hayo. Wengine wanahoji kwanini bei zinapanda kwa kasi wakati mafuta yaliyopo yalishanunuliwa kabla ya mivutano hiyo kuanza, huku wengine wakikiri kuwa soko la dunia lina mchango mkubwa usioepukika.

Wakati mjadala ukiendelea, athari zimeanza kuonekana moja kwa moja kwa wananchi. Abiria wa usafiri wa umma wanaripoti kupanda kwa nauli katika baadhi ya maeneo, licha ya kuwapo maelekezo ya mamlaka kudhibiti ongezeko hilo.

Ester Jeremia, aliyesafiri kutoka Posta hadi Makumbusho jana, alisema nauli imeongezeka kutoka Sh. 600 hadi Sh. 700. Andrea James wa Tabata Segerea alieleza kuwa nauli ya Segerea-Makumbusho imepanda hadi Sh. 900 kutoka Sh. 700, huku njia ya Kimara-Mnazi Mmoja ikipanda hadi Sh. 1,000 kutoka Sh. 800.

Kwa upande wa vituo vya mafuta, baadhi vimeanza kuweka masharti ya muda kwa wanunuzi.

Fausta Pendael alisema alizuiwa kununua mafuta ya zaidi ya Sh. 10,000 katika kituo cha mafuta, kabla ya kutangazwa kwa bei mpya.

Awali Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia Mafuta na Gesi Asilia, Dk. James Mataragio, alisisitiza kuwa nchi ina akiba ya kutosha hadi Julai, akieleza kuwa mafuta yaliyopo, yanayokuja na yaliyo kwenye mikataba yanatosha kwa zaidi ya siku 90.

**LATRA YAONYA**

LATRA imewaonya vikali watoa huduma za usafirishaji nchini dhidi ya kupandisha nauli kiholela kufuatia ongezeko la bei ya mafuta, ikisisitiza kuwa hatua hiyo itakuwa ni kuwaumiza wananchi bila kuzingatia taratibu na mwongozo rasmi.

Onyo hilo lilitolewa na Mkurugenzi

INAENDELEA UK. 3



Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027, bungeni, jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH



HABARI KITAIFA

# Bei za mafuta zatikisa

INATOKA UK. 2

genzi Mkuu wa LATRA, Dk. Habibu Suluo, jana mjini Kibaha mkoani Pwani, alipozungumza na waandishi wa habari katika semina iliyoandaliwa muda mfupi baada ya kutangazwa kwa kupanda kwa bei ya mafuta nchini.

Dk. Suluo alisema mamlaka hiyo imepokea taarifa kuwa baadhi ya wasafirishaji wameanza kupandisha nauli bila idhini, hatua aliyoitaja kuwa ni kinyume cha sheria na isiyokubalika katika kipindi hiki cha mpito.

"Ninawaomba sana wasafirishaji wasitumie kupanda kwa mafuta kuwaumiza Watanzania. Hiki ni kipindi cha mpito, hivyo hawapaswi kuongeza nauli bila mwongozo wa LATRA," alisisitiza.

Alionya kuwa mamlaka haitosita kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watoa huduma watakaokiuka maelekezo hayo, akieleza kuwa ulinzi wa maslahi ya abiria ni kipaumbele kikuu cha LATRA.

Katika hatua ya kutafuta suluhisho la pamoja, LATRA imeitisha kikao cha dharura kitakachofanyika Aprili 8, kitakachowakutanisha wadau wote wa sekta ya usafirishaji ili kujadili namna bora ya kukabiliana na changamoto hiyo ya ongezeko la gharama za mafuta.

Kwa mujibu wa Dk. Suluo, kikao hicho kitatoa jukwaa la majadiliano ya wazi yatakayosaidia kupata mwafaka bila kuathiri wananchi, huku akisisitiza umuhimu wa wadau wote kushiriki kikamilifu.

"Tunawaomba waje kwenye kikao hicho ili tujadili kwa pamoja namna ya kuvuka kipindi hiki. Hatupaswi kukimbilia uamuzi wa haraka bila kufuata utaratibu," alisema.

Alibainisha kuwa kikao hicho kitarushwa mbashara kupitia vyombo vya habari ili kuwapa fursa wadau wengine na wananchi kufuatilia na hata kutoa maoni yao, hatua inayolenga kuongeza uwazi na ushirikishwaji katika uamuzi.

"Ni kweli kuna changamoto za kimataifa, lakini tusiwaachie wananchi wabebe mzigo huu peke yao. Tunahitaji mshikamano na uwajibikaji katika kipindi hiki," aliongeza.

Alisisitiza kuwa suluhisho la kudumu linapaswa kupatikana kupitia majadiliano na si hatua za haraka zinazoweza kuongeza ugumu wa maisha kwa Watanzania.

**VITUO VYA MAFUTA**

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Vituo vya Mafuta Tanzania (TAPSOA), Mahfudhi Maulid, amesema kupanda kwa bei ya mafuta nchini kunachangiwa na sababu mbalimbali za kimataifa, ikiwamo mivutano ya kisiasa na kiusalama inayoendelea katika ukanda wa Mashariki ya Kati.

Alifafanua kuwa gharama za uzalishaji mafuta katika nchi za Kiarabu zimeongezeka kutokana na athari za vita, hali ambayo imeathiri moja kwa moja bei ya bidhaa hiyo katika soko la dunia. Vilevile, alisema gharama za usafirishaji nazo zimepanda kufuatia ongezeko la viwango vinavyotozwa na meli zinazosafirisha mafuta, sambamba na kupanda kwa gharama za bima ya mizigo (premium).

"Kuna watu wanajiuliza kwa nini bei zinapanda wakati tulisema tuna akiba ya kutosha. Ukweli ni kwamba bei hizi hazitengenezwi nchini. Zinachangiwa na hali ya soko la dunia. Kampuni zinazoagiza mafuta zinanunua kwa bei ya juu zaidi sasa kuliko ilivyokuwa awali," alisema.

Aliongeza kuwa ongezeko hilo la gharama katika hatua zote za mnyororo wa usambazaji, kuanzia uzalishaji, usafirishaji hadi bima. Mnyororo ndiyo unaosababisha bei ya mwisho kwa mlaji kupanda, akisisitiza kuwa wadau wa ndani hawana uwezo wa kudhibiti kikamilifu mabadiliko hayo ya kimataifa.

**BEI NCHI ZINGINE**

Bei za mafuta zinaendelea kupanda katika masoko mbalimbali duniani, zikionesha tofauti kubwa kati ya nchi na kuweka shinikizo kwa watumiaji na serikali katika kusawazisha uchumi wao.

Nchini, hali inaonekana kuwa tulivu kiasi licha ya mabadiliko ya soko la dunia. Kwa mujibu wa EWURA, kuanzia Aprili Mosi, 2026, petroli jijini Dar es Salaam inauzwa kwa Sh. 3,820 kwa lita, huku dizeli ikiwa Sh. 3,806 kwa lita. Mamlaka hiyo pia imeeleza kuwa akiba iliyopo inatosha kukidhi mahitaji ya ndani kwa sasa.

Picha ni tofauti kabisa katika nchi jirani. Malawi, bei za mafuta zimefikia viwango vya juu zaidi katika ukanda huu, huku petroli ikiuzwa kwa takribani Sh. 9,836 kwa lita na dizeli Sh. 9,858, zaidi ya mara mbili ya bei ya Tanzania.

Hali hii inaifanya Malawi kuwa miongoni mwa nchi zilizoathirika zaidi na kupanda kwa gharama za nishati.

Afrika Kusini nayo inakabiliwa na shinikizo la bei, ingawa bado iko chini ya Malawi. Petroli inauzwa kwa wastani wa Sh. 3,541 kwa lita, chini kidogo ya Tanzania wakati dizeli ikiwa Sh. 3,928, juu kidogo ya bei ya Tanzania. Kwa Marekani, soko linaonesha nafuu zaidi kwa petroli inayouzwa kwa takribani Sh. 2,742 kwa lita, huku dizeli ikiwa karibu Sh. 3,717. Licha ya kuwa na bei ya chini, nchi hiyo pia ina faida ya soko pana na usambazaji ulio imara zaidi.

Wataalamu wanaonya kuwa nchi nyingine za Afrika Mashariki zinaweza kukumbwa na hali kama ya Malawi pindi zitakapofanya marekebisho ya bei kulingana na mifumo yao ya ndani.

**HISTORIA YA BEI**

Takwimu zinaonesha kuwa kati ya mwaka 2008 na 2009, Tanzania ilishuhudia kushuka kwa bei za mafuta kufuatia kuanzishwa kwa mfumo wa udhibiti chini ya EWURA. Petroli ilishuka kwa asilimia 14.67, dizeli kwa asilimia 22.63 na mafuta ya taa kwa asilimia 27.21.

Hata hivyo, kuanzia 2009 hadi 2011, bei zilipanda kwa kasi kubwa. Petroli iliongezeka kutoka Sh. 1,379 hadi karibu Sh. 1,998, huku dizeli na mafuta ya taa nazo zikiongezeka kwa viwango vikubwa, hasa mafuta ya taa yaliyopanda kwa zaidi ya asilimia 100, yakichangiwa na ongezeko la ushuru mwaka 2011.

Baada ya 2011, kasi ya ongezeko la bei ilianza kupungua, ikiashiria kipindi cha utulivu wa kiasi hadi mwaka 2012, ingawa viwango vya bei vilibaki juu.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wagombea urais na wagombea wenza kutoka vyama vya siasa 16 vilivyoshiriki Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: IKULU

RIPOTI ZA CAG, TAKUKURU, PPRA:

# Waziri Mkuu aelekeza uchunguzi mkali wa wizi wa mali za umma

Na Rehema Matowo, DODOMA

WAZIRI Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba, ameagiza vyombo vya dola na mamlaka za nidhamu kufanya uchunguzi wa kina na kuchukua hatua kali dhidi ya wote watakaobainika kuhusika na wizi wa fedha za umma, ubadhirifu au vitendo vya hujuma.

Agizo hilo limekuja kufuatia hoja za taasisi za usimamizi na ukaguzi, ikiwamo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), ambazo zimebainisha upungufu katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2026/27 bungeni Dodoma jana, Dk. Mwigulu aliomba kuidhinishwa kwa Sh. trilioni 12.5, ambapo Sh. trilioni 8.73 ni matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 3.76 kwa miradi ya maendeleo.

Alisisitiza serikali itahakikisha hoja zote za ukaguzi zinapatiwa ufumbuzi na maofisa masuuli wanawajibika kwa wakati, ili kuongeza ufanisi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Katika hatua inayotia wasiwasi, Waziri Mkuu alibainisha kuwa watumishi wa umma 7,447 wamegundulika kulipwa mishahara binafsi yenye thamani ya Sh. bilioni 14.34 isiyoendana na majukumu yao.

Kutokana na hilo, serikali inapanga kuhuisha sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma ili kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

Katika kupambana na rushwa, zaidi ya Sh. bilioni 60 zimeokolewa kupitia uchunguzi, huku TAKUKURU ikitakiwa kuimarisha mikakati ya kuzuia vitendo hivyo mapema.

Pamoja na hatua za nidhamu, serikali imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa kupandisha vyeo na madaraja kwa zaidi ya watumishi 662,000, kubadili kada kwa zaidi ya 42,000 na kulipa malimbikizo ya mishahara yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 248. Watumishi wapya 155,008 pia wameajiriwa kuimarisha utoaji huduma.

Katika sekta ya madini, alisema serikali imeendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa mafunzo na kutenga maeneo 99 ya uchimbaji, hatua iliyochangia makusanyo ya Sh. bilioni 771.53, sawa na asilimia 64 ya lengo.

Ili kuongeza tija, sehemu ya mapato ya madini itaanza kutengwa kwa ajili ya utafiti wa utafutaji wa rasilimali hizo.

Sekta ya nishati nayo imepewa msukumo mpya, ambapo serikali inalenga kuimarisha uzalishaji na usambazaji umeme, huku ikihamasisha matumizi ya gesi asilia kama mbadala wa mafuta ya petroli ili kupunguza gharama na utegemezi wa soko la dunia.

Katika kilimo, serikali imepiga marufuku utaratibu wa 'lumbesa' na kuagiza mazao yauzwe kwa vipimo rasmi, huku halmashauri zikikatazwa kutoza ushuru holela. Vyama vya ushirika vimetakiwa kununua mazao kwa fedha taslimu ili kuwalinda wakulima.

Sekta ya utalii imeendelea kuimarika, ambapo idadi ya watalii imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 10, na mapato kufikia dola za Marekani bilioni 4.4.

Katika elimu, serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, vyoo na maabara ili kuboresha mazingira ya kujifunzia.

Kwa upande wa afya, juhudi zinaelekezwa katika kuongeza uzalishaji dawa, kuboresha miundombinu na kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi.

Vilevile, serikali inaendelea kukuza uwekezaji, ambapo miradi 927 yenye thamani ya dola bilioni 11.08 imesajiliwa, huku maeneo maalumu ya uwekezaji yakiboreshwa ili kuchochea uchumi wa viwanda.

Katika kupambana na rushwa, zaidi ya Sh. bilioni 60 zimeokolewa kupitia uchunguzi, huku TAKUKURU ikitakiwa kuimarisha mikakati ya kuzuia vitendo hivyo mapema.

Kwa ujumla, serikali imeweka maeneo 11 ya kipaumbele katika bajeti ya 2026/27, yakilenga kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa tija, ikiwa ni pamoja na kusisitiza uwajibikaji, ulipaji fidia kwa wakati na ubora wa miradi ya maendeleo.

USAFIRISHAJI

# SGR kuunganishwa hadi Burundi, DRC

**Na Mwandishi Wetu,** KINSHASA

NCHI za Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi zimesaini makubaliano ya kuanza ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kilomita 900 kwa ajili ya kuunganisha fursa za kiuchumi na urahisi wa kutembea kutoka eneo moja kwenda lingine.

Uamuzi huo umefikiwa jana jijini Kinshasa wakati wa kikao cha pamoja kusaini makubaliano ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo wa kutoka Gitega-Bujumbura Uvira hadi Kindu.

Kikao hicho kiliongozwa na Naibu Waziri Mkuu wa DRC, Jean Pierre Gombo, na kuhudhuriwa na Waziri wa Uchukuzi Burundi, Damien Niyonkuru na Katibu Mkuu wa Uchukuzi Tanzania, Prof. Godius Kahyarara.

Akifungua kikao hicho ambacho mawaziri wa nchi hizo wamesaini kuanza kwa mradi huo, Naibu Waziri Mkuu wa DRC, Gombo alisema ni kipaumbele cha nchi za Afrika Mashariki zisizo na bahari ambapo kuna manufaa makubwa ya kiuchumi kuunganisha nchi hiyo na Bandari ya Dar es Salaam ambako husafirisha shehena nyingi.

"Mradi huu ni kipaumbele kwa DRC kwa kuwa tunatambua manufaa ya kuunganisha nchi yetu na Bandari ya Dar es Salaam ambako tunasafirisha na kupokea shehena nyingi, ni muhimu katika kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa nchi yetu, kupunguza gharama za usafiri na kuwezesha bidhaa kusafirishwa kutoka eneo moja kwenda lingine," alisema.



Naibu Waziri Mkuu wa DRC, Jean Pierre Gombo (kulia), akisalimiana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara kabla ya kikao cha mawaziri wa nchi za Burundi, Tanzania na DRC kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Alisema inachukua zaidi ya miezi sita mizigo au shehena kutoka Dar es Salaam hadi Jimbo la Kindu, kwamba mradi huo ni suluhisho la matatizo mengi ya uchukuzi kwa nchi hiyo, kwamba ni utekelezaji wa ajenda ya mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika (AU) kuhakikisha nchi zote zinaunganishwa na huduma za uchukuzi.

Gombo alisema vikao mbalimbali vimeshafanyika na kuanisha vyanzo vya mapato, huku akimtaka mkandarasi mshauri kuharakisha upembuzi yakinifu kabla ya Agosti mwaka huu, ili kuanza kutangazwa zabuni na kutafuta fedha ili mradi uanze rasmi Januari 2027.

Waziri wa Uchukuzi wa Burundi, Niyonkuru alisema serikali ya nchi hiyo ipo tayari kutekeleza mradi huo kwa kuwa utaleta mageuzi ya kiuchumi, ikiwamo kuwezesha madini kusafirishwa kutoka nchini humo kwenda kwenye masoko ya Tanzania na duniani kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Kahyarara alisema mradi huo ni wa Reli ya SGR ya kilomita 900 kutoka Burundi hadi DRC, na kwamba ikijumlishwa na iliyojengwa na inayojengwa nchini ni zaidi ya kilomita 6,000.

"Reli hii inelenga kuzinunganisha nchi zisizo na bahari, melekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha nchi zote zinazotumia Bandari ya Dar es Salaam zimeunganishwa na SGR, kwasasa nchi zote zinazotuzunguka zimeona faida ya reli hii, DRC Congo, Burundi wamejiunga na Uganda wataunga kupitia Isaka,"alifafanua.

Aidha, alisema hatua hiyo ina maana kubwa kiuchumi kwa kuwa Tanzania itakuwa lango la nchi zote jirani, itaongeza biashara, itakuza viwanda na kukuza uchumi wa nchi na taifa kwa ujumla.

Alisema mradi huo utaunganisha migodi mikubwa Nikel ya Msongati-Burundi, Mgodi wa Kabanga-Tanzania ambayo imekaribiana na kwamba mkakati wa nchi ni kujenga kituo kikubwa cha kiuchumi eneo la Kahama kwa ajili ya kuongeza thamani madini.

"Uwepo wa reli hii, unaongeza thamani ya eneo la Kahama, lakini kwa kiwango kikubwa tunaona viwanda vya kisasa vya kuchakata madini ya kimkakati ambavyo wawekezaji wanaona umuhimu wa kuvijenga eneo la Kibaha ambako kuna eneo la viwanda Kwala ambalo nchi zote zenye madini zinahifadhi. Ndani ya muda mfupi Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kuzalisha betri za magari ya umeme, bodaboda na sola," alifafanua.

Kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi hiyo, alisema nchi hizo zimejadili kwa kina na kukubaliana kutotegemea njia zile zile za kupata fedha za miradi, bali kutumia kampuni kubwa za madini, kampuni kubwa za meli duniani zinazotumia Bandari ya Dar es Salaam ambazo zimeonesha nia ya kuwa sehemu ya miradi ya uchukuzi.

"Tunakuja na mkakati wa kuhamasisha upatikanaji wa fedha wa ubinifu. Mfano Bandari ya Dar es Salaam kuna wawekezaji wakubwa kama kampuni ya meli inayojenga gati mpya katika Bandari ya Kigoma, pia wanajenga Bandari ya Karemii upande wa DRC, pia kampuni za madini zinajenga kilomita 400 hadi 500 za barabara kwa kiwango cha lami kutoka Manono hadi Karemii-DRC," alifafanua.

**UMUHIMU WA PPP**

Kuhusu umuhimu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Prof. Kahyarara alisema manufaa yameshaonekana kupitia uwekezaji uliofanywa na DP World katika Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema ubia huo umewezesha Mamlaka ya Bandari (TPA) kuwa na fedha za kutekeleza miradi 22 ya ujenzi wa bandari zote za maziwa makuu kwa fedha zao.

Mkurugenzi anayesimamia kitengo cha kudhibiti vihatarishi wa Benki ya Azania, Lukwaro Semkiwa alisema ni benki ya mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo ni imara na iko tayari kutekeleza miradi ya kimkakati.

"Sisi na mifuko ya hifadhi ya jamii tunashiriki ana katika miradi ya kimkakati ya serikali, na tumeshirikishwa katika mradi wa SGR kuunganisha Tanzania, Burundi na DRC. Tumejidhatiti kushiriki na tutaandaa namna ya kupata mtaji mkubwa kupitia masoko ya hisa, ili tutoe hati fungani maalum kwa ajili ya kujenga SGR hii. Tunaamini utakuwa ni uwekezaji manufaa kwa umma,"alisema.

Mwakilishi wa Sekta Binafsi, Mahfudhi Mazrui alisema wanaona fursa kubwa kibiashara kwenye usafirishaji wa mafuta kwa kuwa inachukua wiki mbili hadi tatu kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam hadi DRC, lakini kwa SGR itakayojengwa itachukua siku mbili hadi tatu kufikisha shehena.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji wa Usafirishaji wa Ushoroba wa Kati, Wakili Pierre Okandju Okonge alisema taasisi hiyo ni kwa ajili ya unaunganisha nchi saba kwa lengo la kurahisisha biashara, usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salama kwenda nchi zisizo na bandari, kuimarisha miundombinu ya kikanda kwa kushirikiana na wizara za uchukuzi na forodha.

Gavana wa Jimbo la Maniema, Mussa Kabwankubi, ambako mradi wa SGR utafika eneo la Kindu, alisema manufaa ya kiuchumi ni makubwa kwa kuwa wananchi watafanya biashara kwa urahisi, watasafiri na kusafirisha shehena kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi DRC.

Sanlam | Allianz

## TAARIFA KWA UMMA



Witness Johnson Chao



Jenipher Shella Jackson

Kampuni ya SanlamAllianz Life Insurance Tanzania Limited inapenda kuutarifu umma kwamba ndugu **Witness Johnson Chao** na ndugu **Jenipher Shella Jackson,** wanaonekana pichani sio wafanyakazi wa Sanlam Allianz Life Insurance Tanzania Limited na hawaruhusiwi kufanya biashara au kuingia makubaliano yoyote kama wawakilishi wa kampuni.

Ajira ya ndugu Witness Johnson Chao ilifikia ukomo mnamo tarehe **10 Februari 2026,** wakati ajira ya ndugu Jenipher Shella Jackson ilifikia ukomo mnamo tarehe **1 Januari 2026.**

Kampuni itaendelea kuwahudumia wateja wote waliokuwa wakihudumiwa na Ndugu Witness Johnson Chao na Jenipher Shella Jackson na haitahusika au kuwajibika na makubaliano, malipo au biashara yoyote itakayofanywa na watajwa hapo juu baada ya kuondoka SanlamAllianz Life Insurance.

Ili kufanya mawasiliano na malipo kwa kampuni yetu, wateja wanashauriwa kutumia mifumo rasimi ya kampuni itumikayo kuwasiliana na kufanya malipo.

**Sanlam Allianz Life Insurance Tanzania Limited**
**Ghorofa ya 9, Amani Place, Mtaa wa Ohio, Dar es Salaam, Tanzania**
**S.L.P 22229 Dar es Salaam, Tanzania**
**+255 22 2127 151-3**
**0800750234**
**Barua pepe: lifeinsurance@sanlamallianz.co.tz**
**Imetolewa na :**
**Sanlam Allianz Life Insurance Tanzania Limited**